BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 29 Februari, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Taarifa ya Hali Halisi ya Dawa za Kulevya kwa mwaka 2022/2023.

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) na iliyokuwa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kwa mwaka 2020/2021.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusumamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Taarifa ya Hali Halisi ya Dawa za Kulevya kwa mwaka 2022/2023.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) na iliyokuwa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kwa mwaka 2020/2021.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi wa Uwekezaji:**

152. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kuna mifuko mingapi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na kwa kiasi gani inasaidia katika kuwakomboa wananchi kupambana na hali ngumu za maisha.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

7. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Fedha na Mipango.

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kutekeleza Miradi mikubwa ya barabara, hospitali na skuli. Ili kuimarisha Demokrasia na Utawala Bora nchini Miradi hiyo iliyotekelezwa inapaswa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Hata hivyo, Ofisi hiyo bado inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa fedha na kushindwa kutekeleza shughuli zake kikamilifu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuitengea fungu maalum la fedha ofisi hii kwa ajili ya kufuatilia miradi hiyo kwa wakati.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

92. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na uhaba wa vyuo vya kufundisha walimu wa vyuo vya ufundi.

Je, Wizara ina mikakati ipi ya kupambana na changamoto hii.

140. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali imejitahidi kuanzisha Vyuo vya Amali Unguja na Pemba ili kuwasaidia vijana kupata stadi za ufundi zinazohitajika katika soko la ajira na kujiajiri. Hata hivyo, vyuo hivi vinakabiliwa na changamoto nyingi katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

(a) Je, ni vipi kozi zinazotolewa na vyuo hivi zinawawezesha wanafunzi kujiajiri na Serikali inatoa msaada gani kwa wanafunzi waliohitimu ili kuwawezesha kujiajiri.

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa vijana waliohitimu kozi katika vyuo vya amali lakini wanashindwa kuendelea na masomo ya vyuo vyengine kwa sababu kozi hizo hazitambuliwi na taasisi za NACTE na TCU.

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha vyuo hivi vina vifaa vya kutosha katika mafunzo maalum 'workshop' zao ili ziweze kusaidia wanafunzi kujifunza kwa vitendo.

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

66. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Katika kuulinda utamaduni na silka za watu husika, kuna mambo manne muhimu yanayohitaji kutunzwa na kutochezewa ambayo ni mavazi, chakula, dini na lugha. Hata hivyo, mwelekeo wa Zanzibar unaonyesha kwamba umuhimu wa mambo yote manne hayo umesahauliwa na Serikali.

(a) Je, ni utaratibu upi unaotumika na Serikali kuhakiki usahihi na viwango vya nguo zinazoingia Zanzibar kulingana na ustaarabu na utamaduni wa Zanzibar.

(b) Kwa kuwa kuna maduka mengi ndani ya Zanzibar yanayouza nguo ambazo ziko kinyume na utamaduni na silka za Mzanzibari, Je, ni utaratibu upi wa kuyapatia ruhusa maduka kama haya.

(c) Je, ni mkakati upi wa Serikali wa kutunza utamaduni na silka za Zanzibar kupitia mavazi, chakula, dini na lugha.

130. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Moja ya malengo ya kuulinda na kuuhifadhi utamaduni wetu ni wazo la kuwa na jengo la utamaduni jumuishi (Cultural Complex Building).

Je, Wizara yako imefikia wapi katika kuona wazo hili linatekelezeka kwa maslahi ya kuuenzi, kuulinda na kuuhifadhi utamaduni wa Mzanzibari.

169. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Katika miaka ya hivi karibuni, mavazi ya kubana na ya nusu utupu wanayovaa akina mama na wanawake wengi hapa Zanzibar, yameenea majiani na sehemu mbali mbali za wazi. Mavazi hayo yanakiuka utamaduni wa Zanzibar na yanapelekea kukithiri kwa matendo mbali mbali yenye kuvunja Sheria na Shariah.

(a) Je, Wizara yako imechukuwa hatua zipi kukemea na kupiga vita mavazi hayo.

(b) Je, Wizara yako imefanya tathmini yoyote na kujua mavazi hayo yanavaliwa na wanawake wa Kizanzibari au ni wepi.

(c) Je, Wizara yako imefanya tathmini ya kujua kwa kiwango gani wanawake wa Kizanzibari wameanza kuiga utamaduni huu mbaya wa kuvaa mavazi yasiyo na staha.

<u>**Wizara ya Afya:**</u>

82. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutujengea hospitali ya kisasa katika Wilaya ya Kitogani. Wakati ilipofunguliwa hospitali hiyo, tuliambiwa kuwa patakuwa na huduma ya kampuni ya usafi kwa ajili ya kuboresha mazingira katika hospitali hiyo.

(a) Je, kwa kiwango gani unalifahamu suala hili.

(b) Je, ni lini hospitali hiyo itapatiwa wahudumu wa usafi.

(c) Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na huduma ya usafi kwa hospitali hiyo.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

13. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto inayowakabili wakulima katika bonde la Dobi Wawi.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

34. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Barabara ya Chake Chake – Wete imeanza kutengenezwa kwa muda mrefu sana lakini hadi leo hii bado haijakamilika.

    (a) Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya kucheleweshwa ujenzi wa barabara hiyo.

    (b) Je, tatizo ni lipi lililopelekea kucheleweshwa ujenzi huo.

160. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Ukosefu wa viwezeshaji katika mifumo ya usafiri wa umma, umekuwa ni changamoto ya muda mrefu kwa jamii ya watu wenye mahitaji maalum.

    Je, ni yepi matarajio ya wananchi kwa siku zijazo, hasa wenye mahitaji maalum kupata huduma hiyo kwa ufanisi kama wanavyopata watu wengine.

171. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Pamoja na sababu mbali mbali zinazopelekea ajali nyingi za barabarani, inafahamika wazi kuwa, madereva walevi wanaoendesha vyombo vya moto wakiwa wamelewa, wanachangia kuongezeka sana kwa ajali hizo.

    (a) Je, Wizara yako imefanya tathmini yotote kujua ni madereva wangapi walioendesha gari huku wamelewa kwa mwaka 2021/2022.

(b) Je, hatua zipi za kisheria zimechukuliwa dhidi ya madereva hao.

(c) Je, kwa nini Serikali haipigi marufuku na kuzuia kabisa matumizi ya vileo hapa Zanzibar.

## IV. TAARIFA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Taarifa ya Hali Halisi ya Dawa za Kulevya kwa mwaka 2022/2023.

## V. HOJA ZA SERIKALI

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) na iliyokuwa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) kwa mwaka 2020/2021.

**Zanzibar,**
**29 Februari, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**